



Wimbo niupendao




Tusome Early Literacy Programme

Wimbo niupendao



Kila asubuhi nikiamka, mama
huniwekea maji ya kuoga bafuni.
Mama huniambia, ni vizuri kuoga.
Mtoto safi hapati magonjwa.

Kwanza, mimi husafisha kinywa kwa kupiga mswaki.
Ninatumia mikono kuoga.
Ninasugua mwili wote kuanzia kichwa, tumbo hata magoti.






Nikimaliza kuoga, mimi huchana nywele kisha hunywa chai.

Baada ya kunywa chai, mimi huweka mkoba wa vitabu mgongoni.

Kisha humuaga mama na kwenda shuleni.

Mimi na rafiki zangu hutembea hadi shuleni.
Sisi hutembea kando ya barabara kwa uangalifu.
Hatuchezi barabarani.





Kabla ya kuingia darasani, mwalimu huangalia kama tumechana nywele.


Mwalimu pia huangalia kama kucha zetu na nyuso ni safi.

Akimaliza, sisi huingia darasani.

Darasani, sisi huimba wimbo wa sehemu za mwili.

“Kichwa, mabega, magoti, miguu, magoti miguu,
magoti miguu.”

“Kichwa, mabega, magoti, miguu, macho, pua,
masikio na mdomo.”





Baada ya wimbo, sisi hujibu maswali machache kama vile:


Sehemu ya nyuma ya kichwa huitwaje?

Tunatumia sehemu gani kupumua?

Saa nne ikifika, sisi
huenda uwanjani
kucheza mpira.

Sisi hupiga mpira kwa
miguu, kichwa, magoti
na hata mgongo.

Sisi sote hufurahia.



Maswali

1. Mama hufanya nini kila asubuhi?
2. Mimi hufanya nini nikimaliza kuoga?
3. Mwalimu hufanya nini kabla hatujaingia darasani?
4. Tunatumia sehemu gani kupumua?
5. Tunatumia sehemu gani kupiga mpira?

Wimbo niupendao

Hadithi hii inahusu msichana anayependa kuimba wimbo wa sehemu za mwili. Yeye huamka kila asubuhi na kujitayarisha kwenda shuleni. Shuleni, mwalimu wao huwaongoza kuimba wimbo aupendao.



Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.